

Namna ya Kufanya Maombi katika makundi Madogoⁱ

Utangulizi: "Kuunganika katika Maombi" ni njia ya kuhamasisha watu kuunganisha sauti zao katika maombi ya hadhara. Ni wazi kutoka kwenye kitabu cha Matendo kwamba mara nyingi waumini wa awali waliomba pamoja. Ni kweli, kila mmoja wetu anahitaji kuomba binafsi, na maombi yetu kamwe hayapaswi kufanywa kwa "maonyesho," lakini kuna nguvu ya pekee katika maombi kadri tunavyosogea pamoja. (Hii haizuii mtu mmoja kuomba tunapokuwa katika kundi), lengo kubwa hapa ni kumpatia kila mmoja ujasiri wa kuomba anapokuwa na watu wengine na kumshirikisha kila mmoja badala ya mtu mmoja kuonekana ndiye mwombaji maarufu siku zote.

Tunapojifunza maombi katika Biblia, ikiwemo Sala ya Bwana, tunagundua kwamba kuna sehemu mbalimbali za maombi ambazo zote ni muhimu. Sehemu hizo zinafupishwa kwa neno moja la kiingereza "ACTS" yaani MATENDO. Nazo ni:

1. 'Adoration and Praise to God' - **Sifa kwa Mungu**

Ibada na Sifa kwa Mungu: Yeye ndiye Muumbaji na Mpaji wa uhai, Mwokozi wetu.

2. 'Confession to God' - **Maungamo kwa Mungu**

Kuungama kwa Mungu: Yeye ndiye anaye tusamehe na kutuosha dhambi, lakini tunahitaji kuungama dhambi zetu, za binafsi na za pamoja. (Katika maombi ya hadhara si dhambi zote za binafsi zinaweza kuungamwa).

3. 'Thanksgiving' - **Shukrani kwa Mungu**

Kushukuru: Kumshukuru Mungu kwa mibaraka yote tunayopokea kutoka kwake kila siku.

4. 'Supplication or Requests' - **Maombi au Kusihii kwa Mungu**

Kusihii au Kuomba: Mungu ameahidi kutupatia mahitaji yetu na anatusihii kupeleka mahitaji yetu mahususi kwake.

Hatua za Kuongoza "Kuunganika katika Maombi"

1. Kati mfumo huu wa maombi, wote wanaomba pamoja katika kundi, kwa sauti na kwa kupeana nafasi ili kila mmoja aombee kipengele alichopewa kwa kupeana nafasi. Tazama mfano mwishoni.
2. Elezea kwamba tutagawanya maombi yetu katika vipengele vinne. Tutaelekeza maombi yetu katika kila kipengele kwa mada hiyo husika. Hii ni tofauti na tunavyoomba kila siku - mara nyingi huwa tunaombea kila kitu kwa ombi moja.
3. Tutaomba kwa ufupi, maombi ya sentensi katika kila kipengele.
4. Elezea kwamba kiogoz iatatambulisha kila kipengele kwa wimbo mfupi na fungu la Biblia. Kisha utaacha nafasi kwa kila mmoja kuombea mada hiyo husika.
5. Mwisho wa kipengele cha mwisho, kiongozi atafunga kwa "Amina" ya mwisho.

Mfano wa kundi lenye watu wane wanapoomba maombi ya Kikundi: Mtu wa 1: Mungu tunakusifu kwa kuwa Wewe ni mpaji wa uhai; kwa sababu wewe ni Mtakatifu na kwa sababu umejaa rehema. 2: Bwana tunakushukuru kwa kutupatia siku hii ya maombi, kwa neema yako ya baraka zako. Mtu wa 3: Ee wetu, Mungu tunaungama dhambi zetu kila mmoja alizokutenda kwa wazi au kwa siri, tunakuomba utusamehe 4. Mtu wa 4: Ee Mungu wetu, tunakuomba utuondolee janga la Corona na tunakuomba utulinde. Pia tunaomba siku ya leo utuongoze kulisoma neno lako na kulielewa. Kiongozi atahitimisha, Mfano: Tumeomba maombi haya kwa Jina la Yesu, AMINA.

ⁱ Mwongozo huu, umetoka katika Kitengo cha Global Mission GC 2019 | Zipo Sababu muhimu za Kibiblia za kwa nini maelekezo yametolewa kama yalivyo. Kwa semina kamili na maelezo haya tembelea:

<https://netc.adventistafrica.org/huduma> kisha nenda chini kabisa kwenye kipengele cha "**Miongozo mbalimbali**."